# KWENYE TUKIO LA MAADHIMISHO YA MIAKA MIA MOJA YA KUPAA KWA ‘ABDU’L-BAHÁ

Pongezi kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu

Karne moja sasa imepita tangu roho bora ya ‘Abdu’l-Bahá imepaa kuelekea makazi yake ya milele. Kuzaliwa kwake kulitokea sambamba na alfajiri ya Zama za Kishujaa za Imani, na kuondoka Kwake kuliashiria kutua kwa jua la muhula wake wa mwisho. Hakuna onesho la wazi zaidi linaloweza kufikirika kuliko jinsi Yeye alivyodhihirisha nguvu za umoja wa muonekano wa mazishi Yake, ambapo umati mkubwa sana wa waombolezaji kutoka kila dini iliyomo katika nchi walikusanyika pamoja kuomboleza juu ya hasara yao wote. Katika wakati Wake, marafiki wengi walioikumbatia Imani walifyonza roho ya mafundisho matukufu kwa tendo la kumtazama tu Yeye; hadi leo, kama sisi tukitaka kuweka maisha yetu sambamba kwa roho ileile, sisi lazima tuutazame mfano ulowekwa na Bwana, Ambaye neno na kitendo Chake viliakisi mng’ao wa mwanga uliong’aa kutoka Ufunuo wa Bahá’u’lláh.

Kwa kila namna, mfano Wake ni muhimu kwa utambulisho wa Mbahá’í.  Kila Mbahá’í aweza kumgeukia Yeye kwa ajili ya kuelewa vizuri zaidi jinsi ya kueneza mwangaza wa Imani na kwa ajili ya kupata kiolezo cha kufuata wakati tunajitahidi kuamsha mawazo bora ya kiroho ndani ya wale kunaokutana nao. Ushauri Wake mwenyewe, kwamba mwalimu sharti awe “amewashwa kikamilifu” ili kauli yake iweze “kuwa na matokeo”, na wakati huo huo “mwenye kujififisha kabisa na asiye na majigambo” ili “aweze kufundisha kwa lahani ya Umati wa juu”, waweza kufanikishwa katika masimillizi yasiyohesabika ya nafsi za kiroho zilizobadilika kutokana na ukaribu wao kwa ‘Abdu’l-Bahá. Masomo ya kujifunza hayahesabiki kutokana na jinsi Yeye alivyowasilisha mafundisho matukufu kwa kila aina ya mtu, na daima kuendelea kupanua wigo wa umoja, bila kujali utofauti wowote wa muonekano wa nje, lugha, desturi au itikadi.

Ukamilifu wa upendo Wake ulizalisha jumuiya ambayo, hata kwa wakati ule, ingeweza kudai kuwa imetokana na sehemu zote za jamii. Upendo Wake uliwahuisha, uliwatunza, uliwahamasisha; uliondoa umbali na uliwakaribisha wote kwenye meza ya karamu ya Bwana. Kila jitihada ya kujenga jumuiya inayofanyika sasa, kila shughuli ya kielimu na kila juhudi ya kuwafikia watu hubeba matumaini ya kuwasiliana, kupitia juhudi zetu wenyewe, alama ya upendo huohuo ambao Yeye alimimina juu ya kila mtu. Juhudi hizi ni pongezi bora kabisa Anazoweza kupewa, katika maadhimisho haya ya miaka mia na kila siku inayofuata.

Tunamshukuru Bahá’u’lláh kwa kuuletea ulimwengu siyo tu mafundisho Yake, kiwango cha utakaso, ujitoaji, na ukweli, ambavyo nafsi za kiroho daima vinaweza kuvitamani, bali pia, katika umbo la Bwana, mfano usio na kasoro wa jinsi ya uishi maisha ya kiwango hicho. Wakati jamii ya wanadamu inakabiliwa na janga baada ya janga, jumuiya ya Jina Kuu Kabisa, ambayo haiwezi kuepuka kuyaona machafuko kama hayo, ina bahati ya kuwa na kiolezo cha ‘Abdu’l-Bahá mbele yake. Siyo hatari wala vikwazo vinavyoweza kumzuia kutimiza dhima Yake, kama ni kwa kushughulikia mahitaji ya wakati huo au kuandaa kwa ajili ya siku zijazo; siyo chuki wala matukio ya ulimwengu vinavyoweza kumuondoa kwenye njia Yake. Tulivu, mwenye kujiamini na aliyedhamiria, Yeye hakusumbuliwa na vikwazo, akikaribisha shida na taabu katika njia ya Mungu. Mashambulizi dhidi Yake yalikuwa makali yalioje ulisikitishaje mzigo alolazimika kuubeba! Tunakumbuka ushahidi wa dada Yake muadhama, Jani Kuu Kabisa, kwamba “katika

giza la usiku, kutoka vina vya kifua Chake, ilisikika sauti Yake ya kite chenye kuchoma, na palipo pambazuka, muziki mtamu wa ajabu wa ibada Yake uliinuka juu kwa wakaazi wa milki ya juu."

Upitaji wa wakati haujapunguza mshangao wetu tunapotazama "nafasi na tabia ya Yule Ambaye siyo tu katika Kipindi cha Bahá'u'lláh bali katika uwanja mzima wa historia ya kidini, anatimiza kazi ya kipekee." Na kama Shoghi Effendi alivyothibitisha zaidi juu Yake,

> Yeye ni, ndaima ataendelea kuchukuliwa kuwa, kwanza kabisa, kama Kitovu na Mhimili wa Agano usiokuwa na kifani na ukumbatiao vyote wa Bahá'u'lláh, Kazi Yake iliyotukuka kabisa, Kioo cha mwangaza Wake kisichokuwa na mawaa, Kiolezo kamili cha mafundisho Yake, Mfafanuzi Asiyekosea wa Neno Lake, umbo la kila fikra ya Kibahá'í, umbo lililopewa mwili la kila sifa njema ya Kibahá'í, Tawi Lenye Uwezo Kabisa lililochipua kutoka Mzizi wa Kale, Tawi la Sheria ya Mungu, Kiumbe "Ambaye kumzungukia Yeye majina yote huzunguka", Kamani kuu ya Umoja wa Jamii ya Wanadamu, Bendera ya Amani Kuu Kabisa, Mwezi uzungukao Tufe Kuu la Maongozi haya matakatifu kabisa—mitindo na nyadhifa zinazoeleweka na ambayo hupata uelezaji wa ukweli kabisa, wa juu kabisa na bora kabisa ndani ya jina hilo la ajabu la 'Abdu'l-Bahá. Yeye ni, juu zaidi na mbele kabisa ya majina yote haya, "Siri ya Mungu"—msamiati ambao kwa huo Bahá'u'lláh Mwenyewe alichagua kumuita Yeye, na ambao hauturuhusu kumpa nafasi ya Utume, unaonesha jinsi katika umbo la 'Abdu'l-Bahá tabia zisizopatana za asili ya kiutu na ujuzi uliokuwa mkubwa zaidi kumpita mtu na ukamilifu vimeunganishwa na kupatanishwa kwa ukamilifu.

Wafanyakazi wenzangu wapendwa: Sisi tumewakaribisha hapa siyo tu kuenzi kumbukumbu ya 'Abdu'l-Bahá na kuumbuka majaribu Yake na ushindi, bali pia, pamoja nasi, kujidhatiti tena na jumuiya mnazowakilisha kuitumikia kwa dhati Hoja ambayo Yeye ameitumikia kwa kujitolea maisha Yake yenyewe. Katika kutimiza kazi takatifu iliyokabidhiwa na Mzuri Aliyebarikiwa, Yeye aliupa ullimwengu wa Kibahá'í ulinzi wa Mikataba miwili ambayo imeongoza ukuaji na maendeleo yake tangu wakati huo. Mmoja ulikuwa Nyaraka Zake za Mpango Mtukufu, ambao kupitia humo Neno la Mungu limeweza kutangazwa katika kila nchi; na wa pili ni Wasia na Agano Lake, ambao ulianzisha mchakato kwa ajili ya usitawishaji wa Utaratibu wa Kitawala. Sasa, kwenye mwisho wa karne ya kwanza ya Zama za Utungo, na kwenye mwanzo wa mlolongo wa Mipango ya kidunia, uchapuzaji wa maendeleo ya Mpango Mtakatifu wa Bwana unaonekana wazi. Ukunjukaji endelevu wa Utaratibu wa Kiutawala katika kipindi cha miaka mia iliyopita unaoneshwa na uwepo wa asasi nyingi na mawakala kuanzia kwenye ngazi ya kimataifa hadi kwenye ngazi ya vijiji, ambavyo vinapeleka roho ya Imani na kuongoza na kuhimili juhudi za jumuiya ya Wa-Bahá'í ya ulimwengu mzima. Agano ambalo 'Abdu'l-Bahá ndiye alikuwa Kitovu chake linaendelea kuwa ng'ome isiyoingilika. Sisi tunafurahi kuona jinsi Agano linavyomwelekeza kila muumini kuelekea kwa dhima moja ya pamoja, kuhifadhi umoja endelevu unaolea jumuiya inayoendelea kukua ya Mwaminifu. Tukifikiria Uwepo wa Bwana, sisi tunajikuta tumeshikwa na butwa mbele ya mamlaka Yake yaliyozingira kila kitu yaliyoambatana na subira Yake isiyo na kikomo na uelewa Wake, na umakini wa hekima Yake katika kila hali, kwa upole usiokwisha wa uwepo Wake, na upendo Wake bila kikomo ambao uliweza kusikika na kila roho isiyogubikwa. Lakini kila hamasa ya kusifu sifa Zake zisizokuwa na kifani inazuiliwa na kumbukumbu kuwa Yeye hakutafuta sifa wa Umaarufu wa kidunia. Kwa hiyo tunalazimika kushuhudia kuwa: Mpenzi wa mioyo yetu yote, 'Abdu'l-Bahá, kila kitu Chako kilikuwa ni utumishi—utumishi "kamili, uliotakasika na halisi, uliosimikwa uimara, wa kudumu, dhahiri,

uliofunuliwa kwa uwazi na usiohitaji maelezo yoyote”. Tunahifadhi maneno yaliyobaki kwa ajili ya ahadi ya uaminifu Kwako, kwa kiapo chetu kusimamia Agano ambalo Wewe “ulitangaza, ulitetea na kuulinda”, kwa maelezo yetu ya moyo wote ya uaminifu kwa uongozi Wako wa milele na mafundisho Yako, kwa maombi Yako ya dhati na nasaha Zako. Ahadi hii hii inadhihirishwa katika jitihada imara, za kazi ngumu za ulimwengu wa Kibahá’í za kukamilisha dhima iliyokabidhiwa kwake kwa wakati huu. Tukiitazama jumuiya hii inayojitahidi kuishi kwa mfano Wako, inatuvutia kwa maneno Yako yafuatayo:

Enyi marafiki! Mungu ahimidiwe kwamba bendera ya Umoja Mtakatifu imeinuliwa katika kila nchi, na sauti tamu ya Ufalme wa Abhá imeinuliwa kila upande. Malaika mtakatifu wa Umati wa juu anapaza sauti ya “Yá Bahá’u’l-Abhá!” katikati ya moyo wa ulimwengu, na uwezo wa Neno la Mungu unapulizia uhai wa kweli katika mwili wa uwepo.

Kwa hiyo, enyi marafiki waaminifu, inawabidi ninyi nyote kujiunga na ‘Abdu’l-Bahá katika kujitoa dhabihu na katika utumishi kwa Hoja ya Mungu na utumwa kwa Kizingiti Chake kitukufu. Ikiwa mtasaidiwa kufika kwenye fadhila kuu kama hiyo, ulimwengu mzima hivi punde tu utaweza kuwa chombo cha kupokea uzuri ung’aao wa Mungu, na umoja uliotarajiwa kwa muda mrefu wa jamii ya Wanadamu utafunuliwa katika uzuri wote na mvuto katikati ya moyo wa ulimwengu. Hili ndilo tamanio kubwa kabisa la ‘Abdu’l-Bahá! Hii ndiyo shauku kuu ya wale ambao ni waaminifu! Utukufu wa Utukufu wote uwe juu yenu.